

MTIHANI WA MWISHO WA MUHULA WA KWANZA- 2023

KISWAHILI KIDATO CHA TATU

KARATASI YA TATU (FASIHI)

MUDA; SAA $2\frac{1}{2}$

JINA.....DARASA.....NAMBARI.....

MAAGIZO: *Jibu maswali yote katika karatasi hii*

SEHEMU YA A: FASIHI SIMULIZI.

1. a) Eleza umuhimu wa nyimbo katika usimulizi wa hadithi. (al.4)

- **KUburudisha hadhira**
- **Huvuta hisia za hadhira**
- **Huodoa ukinaifu**
- **Husisitiza ujumbe katika hadithi**
- **Huelimisha hadhira. (zozote 4 x 1 = 4)**

b) i) Eleza maana ya misimu. (al.2)

- **Misimu ni misemo inayohusishwa na kundi ndogo la watu na huzuka katika kipindi cha wakati.**

ii) Taja mifano yoyote miwili ya misimu. (al.2)

- **Beste – rafiki**
- **Sare – kubebwa kwenye matatu bila kulipa**
- **Ashuu – shilling kumi**
- **Matatu/ Daladala – gari la uchukuzi wa umma**
- **Boda – pikipiki/ baikeli inayobeba kwa malipo. (mwalimu ahakiki majibu ya mwanafunzi yoyote 2 x 1 = 2)**

c) Taja sifa tatu za vitanza ndimi. (al.3)

- **Huwa kauli zinazokangabya kimatamshi**
- **Huwa ni mchezo wa maneno**
- **Huundwa kwa sauti zinazokaribiana kimatamshi**
- **Hutumia maneni yenye maana zaidi ya majoa au zenye sauti sawa.**

d) Taja sifa tatu za vitendawili. (al.3)

- **Lugha huwa ya kimafumbo**
- **Hutumia lugha ya istiara**
- **Huwa na mianzo maalumu**
- **Aghalabu huegemea mazingira**
- **Huwa fupi (3x1 = 3)**

e) Fafanua umuhimu wa vitendawili. (al.6)

- **Huburudisha hadhira**
- **Huelimisha jamii**
- **Hukuza ewezo wa kufikiri**
- **Huhifadhi historia ya jamii**
- **Hukuza ubunifu**
- **Hutambulisha mazingira**
- **Hukejeli tabia zisizokubalika. (6x1=6)**

SEHEMU YA B: USHAIRI.

Soma shairi lifuatalo kisha ujibu maswali yote.

Akosaye shukurani, zako juhudhi hajali,

Hata nfanyie nini, haoni huyo hajali,

Hata mpe milioni, matusi ndio stahili,

Aona huna akili, ni ye ye ndiye mshindi.

Patia kila la shani, bure unajisumbua,
 Takuona kama nyani, tena atakunyambua,
 Akuona punguani, chochote hutaambua,
 Usingoje shukurana, tenda wema wende zako.

Utafute kwa juhudu, bila kukata tama,
 Mpe apate faidi, wala asipate njaa,
 Hatachoka kukaidi, atakuletea balaa,
 Na mawazo yakuja, maishayo hafikiri.

Mpe vyote nya haluwa, wenzako wamtamani,
 Hatakupa ya muruwa, juhudu haioni,
 Ataka kuzidishiwa, asubuhi na jioni,
 Ufanyacho hathamini, aongeze ya karaha.

Si ndugu wa si mwana, si rafiki si jirani,
 Shukrani kiwa hana, juu uko hatarini,
 Hadharani tatuksana, aulize ndiwe nani,
Ambe kama hajaona, kinyangarika kamawe.
 Hebu yeye msaili, amepata toa nini?
 Haweziye kukubali, kukupa hata thamani,
 Ni bure wake ukali, akutia mashakani,
 Yake wala hayaoni, mwovu hana shukurani.

Mfadili watengaje, jana alikuopoa,
 Mwema wambwekeaje, mabaya wayachokoa,
 Mzazi wadharauje, mbali alishakutoa,
 Sasa jaribu kupo, ujifunze shukurani.

Maswali

1. Lipe shairi hili anwani mwafaka. (al.1)

Mkosa shukurani hajali / mkosa shukurani

2. Hili ni shairi la aina gani? Thibitisha. (al. 4)

Tarbia – lina mishororo minne kila ubeti

Mathawi – lia vipande viwili kila mshororo

Ukaraguni – vin avinambadirika ubeti hadi mwingine

Hutanja (1mk) Kuthibitisha(1mk) 1 x2 =2)

3. Eleza dhamira ya mshairi katika shairi hili. (al. 2)

Tujifunze kutoa shukurani kwa wenzetu waliotutenda mema ili tuimarishe uhusiano mzuri nao.

4. Bainisha mifano mitatu ya uhuru wa mshairi katika shairi hili. (al.6)

- **Inkisari – takuona badala ya atakuona/ maishayo baa badala ya balaa**
- **Tabdila – haluwa badaa yah aula, Muruwa badala ya murua**
- **Kubananga/ kuboronga sarufi – zako juhudu hajali – hajali juhudu zako**
- bure unajisumbua – unajisumbua bure
 - **Utohozi – milioni - million**

5. Andika ubeti wan ne kwa lugha nathari. (al. 4)

**- Hata uki, pa vyovyote vitamu vinavyowafanya wenzako waonee vivu hawesi
 kuonyesha wema wala kutambua juhundi zako. Yeye hutaka kupewa zaidi kila wakati.
 Kila unachokifanya hakithamini bali huongeza usumbufo.**

6. Taja na utoelee mfano tamathali zozote mbili za usemi katika shairi. (al.4)

Tabaine – si rafiki si jirani/ si ndugu si mwana

Tashbihi – takuona kama nyani

Msemo – Tenda wema nenda zako

Balagha – hebu ye ye msaili amepata toa nini?

7. Eleza maana ya neno hili kama lilivyotumika katika shairi hili. (al1)

Shani - ajabu

